

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA

30 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA – TAREHE 30 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini ya Mwaka 2022.

WAZIRI WA NISHATI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

466. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Pugu - Majohe - Viwege njia nne na Kampala - Bwera - Rada hadi Chuo.

467. MHESHIMIWA JANETH MAURICE MASSABURI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuubadilisha Mkoa wa Dar es Salaam kwa kujenga barabara za Mitaa, mifereji na miundombinu mingine.

468. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Mradi wa *TACTIC* utanza Singida Mjini.

469. MHESHIMIWA SAMWEL XADAY HHAYUMA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini barabara ya Hilbadaw – Bashnet itahamishiwa *TANROADS*.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

470. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Viongozi wa Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa wanashiriki mafunzo ya JKT ya muda mfupi.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**471. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM
BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itashawishi Mabenki kufungua Benki nchini Congo DRC katika Miji ya Kalemie na Uvira ili kurahisisha biashara.

WIZARA YA KILIMO:

**472. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP
MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itarejesha kwa Wananchi wa Kata ya Luponde ardhi iliyochukuliwa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Igeri ambayo haitumiki.

WIZARA YA AFYA:

**473. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto ya ukosefu wa dawa kwa Wazee wanaopata huduma ya matibabu bure.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**474. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Jimbo la Igalula.

WIZARA YA MAJI:

**475. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha usambazaji wa maji Mitaa yote ya Kata za Mbezi juu, Wazo na Mabwepande katika Jimbo la Kawe.

**476. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI
(KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatoa bei moja elekezi kwa kila *unit* moja ya maji Wilayani Karatu.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**477. MHESHIMIWA NEEMA GERALD
MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Muswada wa ukomo wa upelelezi wa kesi utaletwa ili kupunguza msongamano wa kesi unaotokana na upelelezi kutokamilika.

WIZARA YA MADINI:

**478. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali haina njia mbadala ya matumizi ya matimba kama ngazi ambayo yanamaliza miti na hivyo kuharibu mazingira.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA
30 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

